Baada ya kuzikwa Rama Daudi aliendelea jangwa la Maoni. Hebu tutazame habari ya kuvutia kwa ufupi iliyoandikwa kwanye sura ileile. Soma 1 Samweli 25.

- Tambua wahusika.
- WhatMaombi ya Daudi yalikuwa ni yapi na jibu la Nabali?
- Abigaili alitikiaje?
- Matokeo ya habari hii ilikuwa ni nini?

**ZOEZI**:

1. Tunajifunza nini kuhusu Nabali (mstari 2-3)?

2. Tunajifunza nini kuhusu Abigaili (mstari 3)?

3. Katika mistari 4-8 Daudi anatuma baadhi ya vijana wake kwa Nabali kuomba. Ni maelezo gani Daudi aliwapa vijana alipowatuma kwa (miatari 5-6)?

4. Sehemu ya pili ya ujumbe wa Daudu kwa Nabali ilikuwa ni nini (mstari 7-8)?

6. Jibu la Dausi kwa ujumbe wa Nabali lilikuwa nini (mstari 12-13)?

___

7. Mmoja wa watumishi alitoa taarifa gani kwa Abigaili, mke wa Nabali (mstari 14-17)?

___

8. Abgaili alichukua hatua. Alifanya nini (verses 18-19)?

___

9. Daudi alimaliza kusema nini tu (mstari 20-22)?

___

10. Abigaili ana nafasi gani kwa Daudi (mstari 23-24)?

___

11. Alipoulizwa alijibu nini juu ya mme wake Nabali (mstari 25)?

___

12. Katika mistari ya 26-31 anaongeaje juu ya Daudi na anafanya rejea gani juu nsfsi yake?

___

## SOMO LA TATU ~ Sehemu 3

**FAFAKARI**:
Kwa muda tafakari juu ya Ibigaili, alisema na kufanya nini. Abigaili hakujinyenyekeza tu kwa Daudi kimwili (mstari 23) alijinyenyekeza pia kwa hali ya uvumilivu. Neno Bwana na mtumishi linaonyesha ni kwa kiasi gani alijinyenyekeza. Angalia neon Bwana wangu limetumiwa mara ngapi katika sehemu hii
_________ Alikuja kwa Daudi kama anayetafuta amani. Alikuwa tayari kubeba lawama za ujinga wa Nabali ili kupunguza shida alitambua nafasi ya Mungu ambayo ilimfanya Daudi asilipe kisasi na kumwaga damu.
. alitoa zawadi zote alizoandaa (matari 18) kwaajili ya Daudi na watu wake.
Aliomba msamaha kwa makosa aliyofanya na kutambua kuwa Bwana angefanya utawala wa Daudi kudumu kwasababu alipigana vita ya Bwana. Japo alikuwa anatafuta usalama kwa Daudi liamkubusha kuwa Bwana angempa usalama. Alimkumbusha Daudi adui zake jinsi alivyomuua Gaoliati kwa kombeo tu. Mwisho akasema kuwa wakati utakapofika atakapoteuliwa kuwa mfalme dhamira yake itakuwa huru kutokana na kushitakiwa na nafsik kwasababu hakulipia kisasi kwa kumwaga damu.

**MASWALI YA MATUMIZI**:
Ni kwa vipi ninatafuta amni na kuepusha hatari kwa kubeba lawama mwenyewe, na hasa matendo na maneno ya muhusika yanapoonekana kuwa ya kijinga?
___

**ZOEZI**:
1. Mwitikio wa Daudi una sehemu tatu ya ukiri wa neema ya Mungu:
a. Mstari wa 32: Kwa Bwana _______________________________________________
b. Mstari waj 33: KwaAbigaili ______________________________________________
c. Verse 34: Of himself _______________________________________________
d. Mstari wa 34: Kwa Nabali na watu wake ___________________________________

Daudi alipokea zawadi yake, akamwambia aende nyumbani, na akamuahidi kumpatia ombi lake (mstari 35).

___

3. Kulitokea nini asubuhi iliyofuata (Mstari 37-38)?

___

4. Habari inaishaje (Mistari ya 39-42)?

___

**MATUMIZI**:
1. Daudi alituma ujumbe kwa Abigaili awe mke wake. Mstari wa 41 unatwambia nini?

___

2. Abigaili ailipokea fursa aliyopewa kuombwa kuwa mke wa Daudi. Alikuwa tayari kumtumikia na kuosha miguu ya watumishi wake. Kwa ufumilivu alijiona mtumishi kwa watumishi wake!
a. Ni kwa vipi maneno na matendo yake vinaenda pamoja na mawazo *ya jamii* juu ya mahusianao ya ndoa?

___

b.Ni kwa vipi maneno yake na matendo yake uanaendana na mawazo yako bianafsi kuhusu amahusiano ya ndoa?

___

## SOMO LA TATU ~ Sehemu ya 3

**UTANGULIZI**:
Ni kwa vipi nafsi itakumbukwa? Taangu kipimdi cha Goliati hadi kufa kwake Sauli hayo yote Daudi alikuwa nayo. Sauli alikuwa mtu aliyeishi kwa hofu na wivu. Alifahamu kuwa Daudi alikuwa na Roho wa Bwana, Roho ambayo wakati fulani ilikuwa yake. Kisha Mungu alichakgua Samweli kumtia matuta kijana mdogo mchungaji Daudi kuwa mfalme aliyefuata. Kwa hasira Sauli alimtafuta Daudi ili auawe na Mfilisti kwatika vita lakini kama mtu mpweke alimshawishi Daudi kumuua hadi hadi kifo chake mwenyewe alipojeruhiwa vibaya na Wafilisti!

**KAZI YA KUFANYA**:
Soma Soma 1 Samweli 31.
**ZOEZI**:
1. Wafilisti walipigana na kushawishi Israeli. Kulitokea nini (mstari 1-3)?
- Kwa Waisrali: ___
- Kwa Yonathani na ndugu zake: ___
- Kwa Sauli: ___

2. Sauli alimwambia mbeba silaha wake kufnyanini (mstaro 4)?

___

Lakini, alikuwa akiogopa na asingetii. Sauli alichagua kufanyaje.?

___

3. Sauli alifariki. Mbeba silah zake aliamua kufanyaje?

Mstari 6 Andika kwa kifupi juu ya kilichotokea siku hiyo:

4. Matokeo ya kushinda kwa jeshila Israeli kulikuwa ni nini na kufa kwa Sauli na watoto wake. (mstari 7)?

5. Mistari 8-10 .inaelezea habari ya kutisha ya vita. Wafilisti walikuja kuteka waliouawa. Walikuta nini?

Walifanya nini?

6. Mwisho watu wa Yabeshi Gilead (Wasisraeli) walifanya nini waliposikia Waisrseli wachomfanyia Sauli (misttari 11-13)?

## KUTAFAKARI:

Hii ni siku ya masikstiko kwa Israele nzima, sauli alikumbukwaje? The Sura za Samweli wa kwanza haitoi sura nzuri ya mtu huyu ambaye alikuwa na kila kitu na bado akafariki bila kitu.
Nguvu ya utu wake kama mfalme na kama kiongozi iliondoka. Watoto wake walifariki. Alikuwa ni picha ya jeshi lililoshindwa aliyekuwa kiongozi sasa amembia mji wake. Wafiisti walishinda Waisraeli , waliwanyang'anya vitu vyao na wakamfanyia mfalme wao na wanawe kama mizoga iliyotundikwa kwanye ukuta wa Beth Shan.
Utawala wa Sauli kwa Israeli ulionyesha siku za giza kwa kushambuliwa kwa ukatili na jeshi la Wafilsiti. Sauli alijua kuwa Bwana alikuwa na Daudi. Alijua kuwa watu wanaimba sifa za Daudi, jasiri wao aliyekuwa na nguvu katika. Bila shaka alama kubwa ya kushindwa kwa Sauli ilikuwa kuchukua upanga wake na kuuangukia.
Sauli alimalizia maisha yake bila matumaini.Ushindi ulikosa. Watoto wake walikufa. Majeshi yake yalikuwa yakikimbia wakiogopa kuuawa na
"Hawa watu wasiotahiriwa [ambao] watakuja na kunikimbiza na kunitukana."

# SOMO LA TATU ~ Sehemu ya 4

## MATUMIZI:

Maisha yanaonekanaje panapokosa matumaini? Maisha yanapokuwa hayana makusudi wala maana, matumaini yako wapi? Kulingalisha kwa watu hawa wawili, Sauli na Daudi, ni kwamba Sauli aliishi kwa matumaini ya kufa kwa Daudi. Daudi kwa upande mwingine, aliishi kwa matumaini ya siku za usoni kwa uhusiano na Bwana wake, Mungu aliyehai.
1. Ninatafuta wapi matumaini? Ninaweka wapi tumaini letu?

2. Ni mjia zipi ambazo maisha yangu yanaonyesha matumaini ya maisha yangu ya baadae?

Kumbuka habari njema ya Mungu kwaajili ya kila mmoja wetu. Nabii Yeremia anaandika katika Yeremia 29:11, "Ninajua mawazo ninayowawazia… mawazo ya kukufanikisha wala siyo kukupa shida, mawazo ya kukupa matumaini siku zoko za mwisho."

Tena katika mstari wa 12 na 13 Mungu anatutia moyo ku ___________________________ juu yangu na
________________________ na ________________________ . Na anaahidi ku
______________________ to you. You will ______________________________ Me and
_________________ Wakati wewe ________________ Mimi na vyote _______________
Ni tofauri gani ambazo lazima ahadi ya Mungu ya matumaini na katika safari ya maisha yajayo hufanya maisha yangu yawe kama ninavyoishi? Sala yangu ya sifa na shukrani ni inakuwa ipi?
___________________________________________________________________________

## KUKARIRI:

Zaburi ya 42 na 43 hurudia mstari mmoja mara tatu. Andika Zaburi ya 42:5a na 11 na Zaburi ya 43:5 kwanye kadi. Umekuwa ukijifunza maisha ya Daudi kama mtu wa vita Na kama mtu anayemkimbia mfalme Sauli. Unaposoma maneno haya sikiliza moyo wa mtunga Zaburi Ni kama anaelezea moyo wa mtu aliyekata tamaa. Soma Zaburi zote mbili na kariri maneno yake.
Wakati mwingine tunaweza kuona kuwa tumetafutwa na maadui wetu pasipomahali pa kujificha. Tunaweza kukata tama na kuvunjiaka moyo. Hii haikuwa tofauti na kwa Daudi. Mtunga Zaburi anatwambia kuwa jibu la kukata tamaa ni kumsifu Mwokozi wetu na Mungu wetu. Andika kwenye kadi maneno yanayokuja kwenye mawazo yako, maneno yanayothibitisha shukrani yako kwa Mungu kwa uwapo wake, ulinzi wake, amani na nguvu katika kazi kwenye maisha yako.
.

## FUNDISHO:

Israeli haina mfalme. Sauli amefariki. Daudi amesikia kufariki kwa Daudi na rafiki yake kipenzi Yonathani.Katika 2 Samweli 2:1 Daudi anamuuliza Bwana atakakokwenda. Bwana anamtuma Hebroni. Anaweka fanilia yake Hebroni. Wanaume wa Yuda wanakuja wanampaka mafuta kuwa mfalme wa Yuda. Sasa chukua nafasi kuonyesha Hebroni kwanye ramani yako. Mji uko kusini mwa Bethlehemu na upande mwa mashariki mwa Bahari ya Chunvi. Ni muhimu kuona kuwa rejea zimefanywa kwaajili ya Israeli na nyumba ya Yuda. Mfano unaonekana katika 2 Samweli 2:4a. “Kisha wanaume wa Yuda walikuja Hebroni na kule walimtawaza Daudi kuwa mfalme wa Yuda.” Kwa kuangalia ramani ambayo inaonyesha mgawanyiko wan chi ya makabila kumi na mawili ni rahisi kuona nchi kubwa aliyopwewa Yuda. Na utagundua kuwa Hebroni iko kwa Yuda. Sasa Daudi alitaka sehemu iliyobaki ya Israeli . Daudi alitaka Israeli wapumzikel, na watu wengine kutoka pande za nchi walikubali awe mfalme wao. Kama mfalme Daudi aliunganisha wananchi na Israeli yote ilibaki ikiwa imeungana katika utawala wa Daudi na mtoto wake Sulemani. Kilichotokea katika sura chache zinazofuata ni mchakato wa kuimarisha daudi katika kiti chake kama mfalme. Mchakato huu ulidai kuondoka kwa na wakati mwingine kufa kwa baadhi ya familia, majemadari wa majeshi yao, na utawala wote. wafalme waliotangulia. Ina maana ya kurithi wajakazi na kuachana na yoyote ambaye anaweza kuwa tishio la utawala. Tutafanya mtazamo wa jumla wa mchakato huu tutakapoangalia sura sita za kwanza za 2 Samweli.

# SOMO LA NNE ~Sehemu ya 5

## KAZI YA KUFANYA:

Soma 2 Samweli 2:4-7. Hii ni jaribiao la kwanza la Daudi la kwanza la kuunganisha nguvu ya kuungwa mkono na watu.

## ZOEZI:

1. Kumbuka mambo ambayo wanaume wa Yabeshi Giliadi waliyoyafanya (1 Samweli 31:11-13).

______________________________________________________________________

2. Daudi alikuwa na ujumbe wenye sehemu tatu kwaajili yao:

- Mstari 5: ____________________________________________________________
- Mstari 6: ____________________________________________________________
- Mstari 7: ____________________________________________________________

## FUNDISHO:

Kiini cha ujumbea wake ni shukrani kwa heshima waliyompa Sauli na na akawaombea Baraka za Bwana kwa waliyoyafanya. Na Mungu akaomba kuwa sawa ana Mungu alivyowaonyesha ukarimu na uaminifu kwamba yeye aliyeitwa Daudi, atafaya vilevile kwasababu ya waliyoyafaya. Mwisho aliwatia moyo watu wa Yabeshi Gileadi kwa kuwapa taarifa kuwa nyumba ya Yuda imemtawaza kuwa mfalme wao.

Ujumbe huu ulikuwa pendekezi la Daudi kwa Waisraeli wa Kaskazini kumpokea kama mfalme wao. Pamoja na hayo, wasomi husema kuwa inawezekanma ilipita kama miaka mitano kbla makabila ya kaskazini kujibu ombi hilo. Katika Dunia hii ambayo mawasiliano ni rahisi mchakato wa kumthibitisha Daudi kama mfalme wao unaweza kuonekana kama jambo lisilo la kawaida na hata la kijinga.

## ZOEZI:

Sasa kuna matatizo, Abneri alikuwa kamanda wa jishi la Sauli na Ish-Bosheth ni mtoto wa Sauli. Abneli Limchukua Ish-Bosheth na kumfanya mfalme juu ya Israeli akijaribu kupitisha ufalme kwa watoto wa Sauli waliokuwa hai (2 Samweli 2:8-11).

1. Vita kati ya nyumba ya Sauli na ya Daudi vilichumia muda mrefu kumalizika (2 Samweli 3:1). Lakini tunaambiwa nini kuhusu nyumba hizi katika mstari wa 1?

______________________________________________________________________

2Abneli aligeuka akamuunga mkono Daudi na kuvunja uhusiano wake na Ish-Bosheth kutokana na mashitaka ambayo Ish-Bosheth alimfanyia Abner (2 Smweli 3:6-11). Yalikuwa mashitaka gani?

______________________________________________________________________

## FUNDISHO:

Mashitaka ambayo Ish-Bosheth alimsema Abner kuwa amelala na kimada Rizpah yalimfanya Abneli ajaribu kumnyang’anya ufalme. Katika mstari wa 6 tunaambiwa kuwa nafasi ya Abeneri katika nyumba ya Sauli ilikuwa ikiongezeka.Ish-Bosheth alikuwa akitishiwa na Abneri. Kuwa hasira Abner aliondoa uhusiano wake na nyumba ya Sauli na kujiung ana Daudi na kuanza kuimarisha ufalme wa Daudi kwa Israeli nzima, kutoka Dani kwenda Berisheba.

## ZOEZI:

1. AbnerI alikuwa ni chombo cha kuleta Israeli wote chini ya utawala wa Daudi (Mstari 12 na inayofuata). Dudi alitka nini kwake (verses 13-16)?

___

2. Yoabu alikuwa kamamda katika jeshi la Daudi. Katika sura ya 2 tunasoma kuwa Abinri alimuua ndugu yake Yoabu. we read that Abner kills Joab's
brother. Kuelekea mwisho wa sura ya 3 tunajifunza kuwa Yoabu anamuua Abineri kulipa kisasi cha damu ya ndugu yake. Daudi hakumlipa kisasi Yoabu kwa kumuua Abineri. Japo mpakwa mafuta Daudi alikuwa bado dhaifu. Anamuuliza nini Bwana (matari 39)?

___

3. Mtoao wa Sauli Ish-Bosheth ameuawa katika 2 Samweli 4 na mwisho katika 2 Samweli 5 Dausi ametambulika kuwa mfalme wa watu wa Mungu.
Anapaswa kutumika ___________________________ kwa watu na alipaswa kuwa
_________________________________________________________________ mstari 2).

4. Ni nani aliyeishi Bethlehemu (mstari 6)?

___

Yesrusalemu ilijengwa kwenye mlima ulioitwa

___

Wayebusi waliamuni kuwa hukukuwa na uwezekano wa Dausi kuteka ngome iliyojengea Sauyni. Mstari wa 7 unatwambia nini?

___

5. Katika mistari ya 9-16 tunajifunza nini kuhusu Daudi?

___

6. Katika sura ya 6 tunasoma juu ya kushangilia kulikotokea Bwana alipoletwa kwenye mji wa Daudi. Ni maneno gani mengine yanayoelezea?

___

7. Daudi aliona nini katika Samweli 7:2?

___

8. Neno la Bwana lililokuja kupitia Nathani (mistari 5-16). Soma mistri hii kwa uangalifu na kwa maneno yako elezea ambacho Bwana alitaka Daudi afahamu.

___

9. Baada ya Nathani kumwambia yote Daudi,Daudi "alikaa mbele za Bwana (verse 18)." Ni mambo gani ambayo Daudi alisema mbele za Bwana?

___

Kumbuka matumizi ya Daudi ya mara kwa mara ya neon mtumishi. Alionaje uhusiano wake na Mungu?

___

10.Utawala wa Daudi umejawa na ushindi. (2 Samweli 8 na 10). Kati ya sura hizi mbili, Tunatambulishwa juu ya sura mpya . Daudi anauliza nini (2 Samweli 9:1)?

___

11. Ziba, mtumishi wa nyimba ya Sauli analetwa kwa Daudi. Anamwambia nini Daudi katika mstari wa
3?_____________________________________________________________________

12. Mephibosheth ameletwa kwa Daudi (mstari wa 6). Daudi alimuahidi nini Mephibosheth?

Alifanyiwa nini  ( mstari 7-13)?

________________________________________________________________

## HITIMISHO:

Ufalme wa Daudi umarishwa na Bwana. Haikuw arahisi na haikutokea kwa siku moja kama tunavyofikiri. Tunamwacha utawala wa Daudi juu katika somo hili. Amepwewa kila kitu na kila alichoomba kilitokea,  "Mini ni nani…na familia yangu ni nini,  kwamba umenifikisha hapa?" Sanduku la agano, uwepo wa Mungu wa kuonekana, ulikuwa Yerusalemu. Amani ilikuwa katika nchi. Maadui zao walishindwa. Mungu aliimarisha Daudi kama mfalme wake na aliimarisha watua wake wa Israeli kama watu wake binafsi. Alikuwa Mungu wao! Mlengo ya Daudi ni kwamba jina la Bwana lingekubwa siku zote. "U mkubwa kiasi gani!

Hakuna kama wewe, na hakuna Mungu isipokuwa wewe…" Sala ya Daudi iwe ni ukiri wako. Ni Mungu wako na ni watu wake. Sifa iwe kwa Mungu utukufu wote na heshima!

# SOMO LA 4 ~ Sehemu 1

## UTANGULIZI:

Habari ya Daudi na Belisheba, sawa na habari ya Daudi na Goliati , zinafahamika vizuri. Umeelezewa katika  2 Samweli 11-12:25. Mungu alimbariki Daudi na mema yake. Yote aliyoota au kutazamia yatokee maishani mwake yaliyotekea. Bwana alifanya Israeli kuwa mshindi juu ya maadui yake. Mungu alipigana vita kwajili ya watu wake. Maisha na muda vilikuwa vizuri!

## KAZI YA KUFANYA:

Soma  2 Smweli 11:1-27.

- Wahusika ni aki na nani?
- Ni mabaya gani yaliyotokea?
- Kivuli kilikuwa ni nini?
- Taarifa ya Yoabu kwa Daudi ilikuwa ni nini?

## ZOEZI:

1. Kilikuwa ni kipindi gani cha mwaka (mstari 1)?

________________________________________________________________

Kulitokea nini katika kipindi hiki cha mwaka?

________________________________________________________________

2. Mfalme alituma __________________________________ pamoja na jeshi la Israeli.
What are we told about David (verse 1)?

________________________________________________________________

3. Daud alikuwa na muda mikononi mwake. Jaribu nini katika mstari wa 2?

________________________________________________________________

4. Berisheba alikuwa ni nani (mstari 3)? Tunajifunza nini kuhusu yeye?

________________________________________________________________

5. Agizo la Daudi lilikuwa ni nini (mstari 4)?

________________________________________________________________

6. Aliletwa kwa Daudi; alilala naye; alikwend nyumbani na ni ujumbe gani aliomtumia (mstari 5)?

________________________________________________________________

7. Katika mstari wa 6 Daudi alimtuma Yoabu kumrudisha Uria Yerusalemu kwake. Baada ya kuuliza vita ilivyokuwa ikiendelea na askari. Daudi anamwambia nini Uria afanye nini (mstari 7-8)?

_______________________________________________________________________

8. Mstari 9 unaanza na neno lakini. Kila kitu kilikwenda sawa na mpango wa Daudi hadi sasa. Lakini nini?

_______________________________________________________________________

9. Ni lini Daudi alimuuliza Uria kwanini hakwenda nyumbani, akifikiri kuwa Uria angelala na mke wake Barisheba, Uria alijibu nini (mstari 10-11)?

_______________________________________________________________________

10. Akiwa amekata tamaa, Alimwambia Uria akae siku nyingine. Alimkaribisha kula na kunywa pamoja naye na kumfanya Uria alewe. Nyingine "lakini" inatokea. Tunaambiwa nini kuhusu Uria katika mstari wa 13?

_______________________________________________________________________

11. Mpamgo wa Daudi wa kwanza ulishindwa. Alimtuma Uria kwa Yoabu na barua. Barua kutoka kwa Daudi lisemaje._

_______________________________________________________________________

12. Kulitokea nin kwa Uria katka mstari wa 16-17?

_______________________________________________________________________

13. Ujumbe wa Uria kwa Daudi ulikuwa ni upi ( mastari wa 18-21)?

_______________________________________________________________________

14. Ujumbe ulitoa taarifa ulielezea yote ambayo Yoabu aliyotumwa kusema. Daudi anapokea ujumbe kutoka kwa Yoabu aliotumwa kusema. Daudi anapokea ujumbe kutika kwa Yoabu na jibu lake ni nini (mstari 25)?

_______________________________________________________________________

15. Sehemu ya habari hii inamalizikaje ( mistari 26-27)?

_______________________________________________________________________

Tunaambiwa kuwa "mambo aliyoyafaya Dausi hayakumpendeza Bwana ."

## KUTAFAKARI:

Wakati hatuwezi kusaidia lolote lakini tunaweza kutafakari kwa yale yaliyotokea tu. Hadi wakati huu Daudi ni muhusika wa mfano kama mfalme. Katika 1 Samweli 13:14 tunasoma kwua Bwana "alitafuta mtu kwa moyo wake na kumteua kuwa kiopngozi wa watu …" Mtu huyu alikuwa Daudi. Sasa anefanya nini? Unasemaje kuhusu habari hii?

_______________________________________________________________________

Tunajifunza nini kuhusu majaribu? Daudi alikuwa na muda mikononi mwake. Alijiruhusu kumtazama Berisheba na kumatamani. Daudi?!? Jasiri wa Israeli na sasa ni mfalme wa Israeli! Mwanamume huyohuyo aliyemabili Goliati , aliyelengwa na mkuki wa Sauli ukutani, na aliyekataa kuua mpakwa matuta wa Bwana alipopewa fursa… Daudi alikuwa ni mtu aliye na kila kitu. Kwanini alishikwa tama kwa kitu ambacho hakikuwa chake, mke wa Uria? Natamaa yake ilimfanya kuzini pamoja naye. Daudi alikosa wake na vijakazi? Tunajua wake zake Mikali na Abigaili.
. 2 Samweli 5:13 inatwambia juu ya wake zake na vijakazi. Daudi kumetokea nini?

_______________________________________________________________________

Jambo moja lilipelekea lingine. Daudi alijaribu kufunika dhambi yake kwahiyo alimwagiza Uria kuja Yerusalemu akiamini kuwa kwavile amekaa muda mrefu angelala na wake. Hiyo

iliposhindwa kutokea Daudi alifikiri kuwa Uria akiwa amelewa angekiuka nia yake. Lakini pamoja hata hivyo haikutokea. Kwahiyo Daudi anapanga kuua! Hata akamfaya Uria abebe kubeba ujumbe wa uria wenye hukumu yake ya kifo. Baada ya kifo cha Uria na muda wa kuomboleza ukawa umepita Daudi namleta Uria ikuru. Anakuwa mke wake n akuzaa mtoto wa kiume.

## SOMO LA NNE ~ Sehemu ya 2

### **FUNDISHO**:

Hebu tuone habari inayofanana nayo. Katika kujifunza Biblia mfururizo wa *Kuifanya Biblia Kuwa Yako*, Somo la pili linaitwa
“Mpango wa Mungu, Chaguo Letu.” Mwanzo 1 na 2 tell inatwambia juu ya yote Mungu aliyoumba na kasha aliwapa Adamu na Eva.
Aliwapa bustani ya Edeni pamoja na yote aliyowapa aliwaamuru kitu kimoja ambacho hawakupaswa kula kilikuwa ni tunda kutoka mti wa mema na mabaya. Lakini tunafahamu jinsi habari ilivyomalizika.Pamoja na yote Mungu aliyowapa waliishia katika majaribu na kuchukua kitu ambacho Mungu hakuwapa, kitu ambacho hakuwapa, kitu ambacho aliamuru walisle. Kila kitu kilikuwa kizuri. Hakuna kitu ambacho kingekuwa bora. Kila kitu ambacho Mungu aliumba kilikuwa chao cha kufurahia. Lakini tunafahamu kuwa mara tu baada ya kutenda dhambi, habari ya kujificha ilianza. Kila mtu alimlaumu mwenzake kwa kile walichokifanya. Walijaribu kujificha. Walikuwa uchi na wenye aibu kwahiyo walijaribu kujifunika kwa majani ya mizeituni. Kitu baada ya kingine kilianza kadiri walivyojaribu kujifunika kwa majani ya mitini. Jambo moja baada ya lingine lilitokea kama matokeo ya dhambi zao. Jambo moja walilojaribu kujificha likuwa ni kuonekana kwao. Dhambi hutuweka mbali na Mungu na kutoka kwa wengine. Dhambi hutufanya kutojikubali aibu yetu wenyewe na ufisadi. Mungu anapotuangalia kwa nje haitaji kutuadhibu. Kinachotokea baadae siyo aibu ya Mungu bali tamko la Mungu juu ya matokeo ya dhambi kwa Adamu na Eva. Adhabu ilikuwa ni kifo lakini habari hiishii hapo. Lakini Mungu aliwarejesha kwenye upendo wake. Anawapa ahadi ya Mwokozi (Mwanzo 3:15) ambaye angebeba juu yake adhabu kwaajili ya dhambi zake, Mwokozi ambaye angewaokoa kutoka mautini na kuwapa uzima wa milele pamoja naye. Tukirudi kwenye habari ya Daudi na Bersheba pamoja na matokeo ya dhambi, na azimio la upendo wa Mungu ambao ulileta kwa Daudi kupitia kwa nabii Nathani.
.

### **KAZI YA KUFANYA**:

Soma 2 Samweli 12:1-19.

### **ZOEZI**:

1Katika mstari wa 1-4 Nathani anamsimulia Daudi hadithi. Kwa maneno yako, hadithi ya Nathini ilikuwa ipi?

______________________________________________________________________________

2. Utafiti wa Daudi katika hadithi ya Nathani ulikuwa ni upi (mstari 5)?

______________________________________________________________________________

3. Daudi aliazimia kuwa matokeo yengekuwaje kwa mtu mtu kama huyo (mstari 5-6)?

____________________________________________________________

4. Kisha Nathani alisema nini,
"__________________________________________________________!"

5.Kisha Nathani alimwambia Daudi ambayo Bwana wa Israeli alisema
a. ______________________________________________________, na
b. __________________________________________________________
c. __________________________________________________________
d. __________________________________________________________

6. Mstari wa 8 unaishaje?

____________________________________________________________

7. Swali la mwisho ni lipi katika mstari 9?

____________________________________________________________

8. Inaonekana kama Bwana anasema, "Daudi, hebu turejee uliyofanya." Maneno ya Nathani kutoka kwa Bwana ni yapi katika mstari wa 9?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

9. Matokeo ya daudi kudhihaki Nono la Bwan na kufanya movu mbele yake ni nini?

____________________________________________________________

10. Mstari wa 11 na 12 ni manenomagumu kusikia. Mungu anamwambia Daudi kitakachotokea. Anakwenda kuleta shida juu ya Daudi. Nini kinakwenda kutokea?

____________________________________________________________

*Kumbuka:* Tutafunza baadae utimilifu wa unabii huu mwishoni mwa somo linalofuata.

11. Daudi anakiri nini kwa Nathani (mstari 13a)?

____________________________________________________________

12. Jibu la haraka la Nathani ni nini (mstari 13b)?

____________________________________________________________

13. Mwisho, ni jambo gani la mwisho la Nathani alilomwambia Daudi kubla ya kuachana (mstari 14)?

____________________________________________________________

____________________________________________________________

14. Mistari ya 15-19 inaelezea juu ya maumivu na masiktiko ambayo yalifuata:

- Kwa mtoto __________________________________________________
- Kwa Daudi ____________________________________________________

____________________________________________________________

- Kwa wazee wa nyumbani kwake _______________________________________
- Kwa watumishi _________________________________________________

## SOMO LA NNE ~ Sehemu ya 3

## KUTAFAKARI:

Ni siku ya mausiktiko kiasi gani. Mfalme mwenye kila kitu amevuliwa heshima na ukuu wake sasa anamwomba Mungu kwa maisha ya mtoto wake.

Anakataa kula anajilaza kifudifudi juu ya ardhi badala ya kulala kwenye chumba chake cha ikulu. Wazee wa nyumba yake wanashindwa kumsaidia. Hawasikilizi watumishi wake wanaogopa kumwambia kuwa mtoto amefariki. Lakini Daudi anajua moyoni mwake kuwa Bwana amefanya

alichokisema kuwa angefanya. Mioyo yetu inauma kwaajili ya baba na mama yake kwa kumpoteza. Tunaweza kufikiri kuwa Mungu alikuwa katili kwao. Tunaweza kusema kuwa msamaha wa Mungu ungejuisha na kumwachia mtoto uhai wake. Nathani alikuja kwake na Bwana akamfanya Daudi kukubali makosa yake. "wewe ni mwanamume!" Daudi alitamka hukumu na adhabu yake mwenyewe. "Lazima alipe kondoo huyo mara mbili zaidi zaidi kwasababu alifanya jambo hilo na bila huruma." Nathani alileta habari mbaya sana:

1. Upanga hautatoka nyumbani kwako.
2. Maafa yatakujia kupitia mtu aliyekaribu na wewe.
3. Mtoto aliyezaliwa kwako atafariki.

Bwana alimleta Daaudi kwenye toba "Nimetenda dhambi mbele za Bwana." Katika mabo yote tunaona kuwa Daudi alifanya makosa. Mwisho tunaona kuwa dhambi inavunja uhusiao wake na Bwana. Je kama Daudi hakuambiwa kukiri kuwa ametenda dhambi kungetokea nini katika uhusiano wake na Bwana? Uhusiano wao ungebaki na kubaki wakiwa wametengana. Lakini Bwana anamujia Daudi akimtafuta, na kuzungumza naye pamoja na dhambi zake, na kumuonyesha udhaifu wake, ili Daudi mwenye dhambi abaki kuwa na heshima yake kwa Mungu kama mtoto wake aliyesamehewa.

## **UTANGULIZI**:

Ndiyo, matokeo ya dhambi. Tunakumbuka katikaMwanzo 2:17 kwamba Mungu aliamuru tunda kutoka la mti kutoliwa na aliwambia Adamu na Eva,
"mkilila hakika mtakufa." Katika Agano tunaambiwa katika Warumi 6:23 that "mshahara wa dhambi ni mauti… Lakini,huo sio mwisho wa habari za Daudi kwetu.

## **KAZI YA KUFANYA**:

Soma 2 Samweli 12:20-26.

## **ZOEZI**:

1. Daudi amethibithiwa kuwa mtoto aliyezaa na Berisheba amefariki.. Baada ya hapo Daudi anafanya nini (mstari 20)?

______________________________________________

2. Unasamgazwa na alichokifanya? Watumishi wake walikuwa. Walimuuliza nini (mstari 21)?

______________________________________________

3. Jibu la Daudi lilikuwa nini (mstari 22-23)?

______________________________________________

4. Daudi na Bersheba walipata mtoto wakiume mwingine (mstari24)?

______________________________________________

5. Lakini Bwana alitaka jina lingine. Alitoa jina gani?

______________________________________________

Kuanzia mstari wa 25 tunajifunza kuwa maana ya jina Jedidiah lina maana gani?

______________________________________________

# SOMO LA NNE ~ Sehemu ya 4

## FUNDISHO:

Siku za furaha zilirejea ikurr. Dudi na Bersheba wanazaa mtoto wa kiume. Wanamwit Selemani. Nathani analeta neno la Bwana kwa Daudi. Anapaswa kuitwa Jedidiah kwasababu amependwa na Bwana. Ni neno la faraja na uthibitisho wa Bwana kiasi gani kuwa amemsamehe Daudi?

Inabidi ifahamike kuwa wajibu aliokuwanao Daudi kama mfalme ni nafasi iliyoleta ategemeo ya ziada kwa jamii. Daudi alikuwa mtu mwenye bahati. Alikuwa ni kila kitu. Mungu alikuwa amempaka mafuta kuwa mfalme juu ya Israeli. Alikuwa amemwokoa kutoka mikoni mwa Sauli. Alimtpa nyumba ya Sauli na wake zake pia. Mungu alikuwa amempa nyumba ya Israeli na Yuda pia. Na alimwambia Daudi kuwa hayo yalikuwa hayatoshi bali angempa zaidi ya hayo.

Kama mtu aliyebahatika na mfalme juu ya nchi yote nchi yote aliyopewa kumwakilisha Mungu katika mambo yake yote. Alipaswa kuongoza watu kama mpakwa mafuta wa Bwana. Kwasababu alikuwa na ushawishi mkubwa, matumaini kutoka kwake yalikuwa makubwa. Alikuwa anastahili kwenye nafasi yake.

Tunaweza kufikiri kuwa adhabu hii ilikuwa kubwa kuliko haki lakini Mungu alitoa kile ambacho kilistahili uovu kwa nafasi aliyokuwa nayo Daudi. Hata Daudi alijua alichostahili. Haki ya Mungu ndani yetu inafahamu haki inapotendeka. Tunafahamu ndani mwetu mtu anapo kwenda pasipokuadhibiwa kwa maovu yake. Tunafahamu pia haki isipotendeka na mtu akiadhibiwa isivyostahili. Tunaweza kufikiri kuwa tusamehe na kusahau lakini lazima kukumbuke matokeo ya tendo kama hilo. Tunapaswa kusamehe, je hiyo inamaanisha kuwa adhabu haistahili au au hakuna matokeo ya maovu? Kumbuka mtoto anayefanya makosa pasipokuadhibiwa. Kutotii, kutachukuliwaje na mtoto huy?

---

Bwana alizungumza kwa ukali kupitia nabii wake Nathani aliposema katika mstari wa 9, “Kwanini ulidhahaki neno la Bwana kwa kufanya yasiyostahili machoni pake?” Unafikiri wakaiti anatuma aletwe Berisheba alijua kuwa anakweneda kinyume mbele za Mungu? Unafikiri dhamira yake ilichagua kudhihaki neno la Bwana? Inaonekana Daudi likuwa na muda mikononi mwake. Watu wake wamekwenda vitani lakini yeye amebaki Yerusalemu. Kutembea kwake juu ya paa la ikulru. Ni usiku wa manane. Hawezi kusinzia. Daudi alikuwa ameshindwa na majaribu kama anavyweza kuwaka silahal zake chini vitani pia hapa alikuwa ameweka silaha zake za kiroho za kupinga majaribu chini.

.

Soma 1 Peter 5:8-9. Kwa kutumia maneno yako, andika Petro anachosema katika waraka huu kwa wakristo.

---

## KUKARIRI:

Hatuwezi kuzungunzia majaribu ya Daudi bila kukumbuka majeribu yetu tuliyonayo katikak maisha yetu. Majaribu ni jambo la kawaida kwetu sote. Hatuwezi kuyaepuka. Yote yametuzunguka. Fahamu kuwa majaribu siyo dhambi bali kushindwa majaribu ndiyo uovu. Kumbuka majaribu ambayo kipekee ni shida kwako. Unaweza kuyaandika katika daftari yako. Yatambue. Yataje kwa majina.Mt. Paulo katika barua yake kwa kanisa la Korintho inasema, “Kwahiyo, ukiwa undhani kuwa umesimama imara, angalia usiangukel!” Angalizo hilo ni

kwaajili yetu sote. Katika kadi yako andika 1 Wakorintho 10:12-13. Mistari hii ina nguvu kwetu. Inatukumbusha kuwa sote tunajaribiwa na tuko kwenye hatari ya kukumbwa na hila za anayezungukazunguka akiaka kutuangamiza. Lakini pia mistari hii inatukumbusha kuwa Mungu ni mwaminifu. Upendo wake unadumu milele. Pia anatutaka kusimama imara kama watu wake. Weka maneno haya kwenye kumbukumbu yako. Uimarishwe na nguvu yake unapotafuta kuimarishwa naye!

**SALA**:
Ee Bwana, Inanipasa kukiri kama Daudi, “Mimi ni binadamu!” Pia nimetenda dhambi. Nimeanguka kwenye njia za hila za mwovu na kugnauka majaribuni za ya ninavyoweza kufikiri. Ninakuja kwako nikiomba msamaha wako kwakuwa ninakuja kwako kwa jina la Yesu. Alikufa ili niweze kuishi na kwasababu hiyo ninakupa shukrani na sifa. Baba ninakuomba uniwezeshe kutawala nafsi yangu na kuwa macho. Uniwezeshe kupinga majaribu, Misha yangu yaonyeshe utakakatifu wako ndani yangu.

---

## SOMO LA NNE ~ Sehemu ya 5

**UTANGULIZI**:
Katika 2 Samweli 12:11-12 Nathani alizungumzia juu ya shida ambayo ingekuja kwa Daudi kupia nyumba yake mwenyewee. Habari inaanzia katika 2 Samweli 13 na inaishia 2 Samweli 18. Hatutasoma habari hii kwa undani bali unahimizwa kusoma sura hizi zote ili upate ujumbe na kufahamu kilichotokea. Habari inahusisha watoto watatu wa Daudi—Mtoto wa kwanza wa Daudi Amnoni, dada yake wa kambo Tamar, na ndugu yake wa kambo Absalom.

**KAZI YA KUFANYA**:
Soma 2 Samweli 13:1-22.

**KAZI YA KUFANYA**:
1. (Mstari 1-2) – Shida ni nini?

_______________________________________________________________________________

2. (Mstari 3-9a) – Yonathani na ni mpwa wake na Daudi, Mjomba wa Amnoni. Amnoni anafuata ushauri gani?

_______________________________________________________________________________

3. (Mistari ya 9b-19) – Amnon alimbaka Tamari na kumtupa nje. Alijihisi kunajisika na kuaibika.
4. (Mistari 20-22) – Absalom anapata habari kutoka kwa dada yake kuhusu kilichotokea na anamfanyia nini?

_______________________________________________________________________________

Absalom hakusema chochote kwa Amnoni, kulitokea nini kwa Absalom?

_______________________________________________________________________________

5. Daudi alipata habari juu ya kilichotokea. Tunaambiwa kuwa alikasirika. Kwa kukosa ndidhamu kwake kulimfanyaje Absolomu?

_______________________________________________________________________________

6. Kulitoea nini katika mstari wa 23-29?

7. Daudi alipokea ujumbe gani (mstari 30)?

8.Yonadabu (tazama mstari wa 3-5) alimwakikishia tena Daudi (verses 32-33).

Absalom alikimbilia kwa babu yake wa upande wa mama yake (1 Nyakati 3:2). Kwa miaka mitatu aliyokuwa kwa babau yake Daudi alimlilia Amnon. Baada ya kufarijiwa alitamani kumuona Absolomu.

## FUNDISHO:

Yoabu , kamanda wa jeshi la Israeli, alijua kuwa Daudi alitaka kumuona Absalom. Aliju pi kuwa Absolom alimuua ndugu yake na kwahiyo haki ilitakiwa kutendeka. Katika sura ya 14 tunajifunza kuwa Daudi alimtuma Yoabu kwenda Geshuri kumrudisha Absalomu Yerusalemu; pamoja na hayo alipelekwa nyumbani kwake wala si kimuona mfalme Daudi.

## ZOEZI:

1. In verses 25-26 we are told about Absalom's appearance. What are we told about him?

2. Katika mstari wa 27 tunaambiwa nini juu ya familia yake?

Absalom alitaka Yoabu ampeleke kumuona babab yake. Yoabau alikataa kuja. Mwisho aliona kuwa njia ya pekee ya kumfany Joabu aone umuhimu aliamua kuunguza shamba lake la shayiri. Alitaka kusema, alifuta hisia ya Yoabu na alipelekwa mbele ya mfalme. (verse 33).

## MTAZAMO WA JUMLA:

Absolomu alianza kuwa na mipango ya hila juu ya Daudi baba yake. Alianza kutumia njia ya kisaikolojia kujivutia watu kwake. Alisikiliza manug'uniko ya watu na kudharau utawala wa baba yake. Alitumia mwonekano wake kuiba mioyo ya wanaume wa Israeli. Ufuasi wake uliongezeka. Ulikua kiasi cha Daudi kukimbia Yerusalemu kumkimbia Absolomu. Daudi aliondoka Absolomu na wafuasi wake walikuja wakauchukua mji. Ahithofel, mshauri wa Absolomu alimshauri kulalala na vijakazi vya baba yake jambo ambalo lilifanyika kwenye hema kwenye paa mbele ya Israeli wote l (2 Samweli 16:20-22). Katika tukio, ushauri wa msahauri wa Absalomu Ahithophel ulivurugwa na ushauri wa Hushai, mmoja wa wapelelezi wa Dudi, ikiwa uta. 2 Samueli 17:14b inasema, “Bwana ameamua kuvuruga ushauri mwema wa Ahithofel in ili kuleta maafa kwa Absolomu.” Daudi na watu wake walisikiliza mipango ya Absolomu ya kushambulia kwahiyo akatuma vikosi chini ya Yoabu., Abishai, na Ittai. Walipotoka kwaajili ya vita,Daudi aliyekuwa amezuiliwa na kuondoka na makamanda aliwaomba kuwa wapole kwa mtoto Absolomu kwaajili yake. Lakini kifo cha Absolomu kilikuwa kinatisha. 2 Samweli 18:9-17 inaelezea habari. Na katika mstari wa 33 tunasikia maombolezo ya Daudi alipolia kwaajili ya mtoto wake Absolomu.

# SOMO LA TANO ~ Sehemu ya 1

## UTANGULIZI:

Habari na simulizi nyingine zimeandikwa katika 2 Samweli 20-24. Daudi alirudi Yerusalemu na kujiimarisha kama mfalme wa Israeli. Watu waliasi, njaa iliikumba nchi, kisasi cha kumwanga damu kiliendelea dhidi ya Wafilisti. Lakini katikati ya haya Daudi alimwimbia Bwana aliyemuokoa kutoka mikoni mwa adui zake wote (2 Samweli 22). Maneno yaliandikwa katika Zaburi ya 18. Mistari ya Zaburi hii inakuwa na maana zaidi tunapogundua maadui wanaotufuatilia. Maadui wa Daudi walikuwa zaidi ya Sauli au Wafilisti ambao walitaka kumuua au kumnyang'anya utawala wake sawa na mtoto wake Absolomu alivyojaribu kufanya. Maadui zake walijumisha hofu, kusumbuliwa na majaribu, kukata tama, na tama. Maadui zake walikuwa zaidi ya nguvu za nje zilizopambana naye. Maadui zake walikuwa na nguvu za mwovu, Yule aliyemtesa Daudi ni yule anayekutesa wewe na mimi.

## KAZI YA KUFANYA:

Kabla ya kuendelea na zoezi, orodhesha kwenye daftari yako maadui wawili au watatu ambao unaweza kuwatambua katika maisha yako. Maadui ni watu wa fujo. Maadu pia ni vitu vinavyo kuzunguka, vinavyo kukabili, na kukusumbua, mawimbi ya uharibifu ambayo yanakufunika , (Zaburi 18:4-5).

## ZOEZI:

1. Daui anatumia lugha za picha katiika wimbo huu (2 Samweli 22). Tambua picha za maneno anazotumia kutoa ujumbe. Bwana ni…

a. Mstari 2 – angu__________________, angu _______________, angu ___________________

b. Mstari 3 – angu _____________________, angu _______________, na ______________

2.Tambua lugha ya picha Daudi anayotumia kuelezea maisha yake Tambuia picha ya maneno anayotumia Daudi kuelezea maisha yake na juhudi za maadui zake zisizochoka.

a. Mstari wa 5 ___________________ ya_________________, ya ________________
_____________________________

b. mstari 6 _______________ ya ___________________, ya _______________
________________________

3. Mstari 4 na 7 tumia fomu ya neno ita, aliita, au alipaza sauti. Umegundua kuwa tunapomuita Bwana kwasababu tunataka kuokoka kutoka kwa maadui wetu kwamba Bwana anajibu? Soma kupitia mistari ya 8-16.

a. Dunia _____________________________ na ________________________________

b. Misingi a mbingu ______________________________________________

"…kwasababu Alikuwa _________________________."

c. Moshi, moto unaounguza, mkaa wenye moto_________________________________________

d. Mawingu ya giza ______________________________________________________________

e. Radi __________________________________________________________

f. __________________________________________________________________________

g. __________________________________________________________________________

h. __________________________________________________________________________

Viumbe vyote vinaitikia hasira yake! Anakuja kutuokoa!

4. Ni picha gani katika mistari ya 17-19!

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

5. Kwanini anafanya “utafiti na kuokoa” kutokana na mstari wa 20?

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

6. Mistri ya 21-25 inaelezea uhusiano wake na sisi. Ametufanya wenye haki mbele zake Ametutakasa. Ametuwezesha kutunza njia zake, kutunza utii kwake.
Ametufanya tubarikiwe, ametulinda na dhambi. Mungu ametulipa sawa na haki yetu. Yeye ni haki yetu!

**MAFUNDISHO**:
Tunahitaji mapumziko kidogo katika masomo yetu kwa soamo la wimbo wa Daudi wa sifa. Tunahitaji tuzungumze juu ya haki. Je sisi tu wenye haki? Bila Mungu siyo. Bibli inafundisha kuwa wote tumetenda dhambi na kwamba hakuna *mwenye haki* hata mmoja. (Warumi 3:10-12). Lakini Daudi alimwamini ahadi za Mungu. Nabii Yeremia anasema, kwamba siku inakuja atakapoinua chipukizi la haki kutoka uzao wa Daudi …na hili ndilo jina atakaloitwa: Bwana *haki yetu* (Yeremia 23:5-6). Na tena, Mt. Paullo anatukumbusha kuwa ni kwasababu ya (Mungu) kwamba uko katika Kristo Yesu, ambaye amekuwa hekima yetu kutoka kwa Mungu—Kwamba ni *haki yetu*, utakatifu, na ukombozi…kwahiyo tunajivuna katika Bwana (1 Wakorintho 1:30-31). Taunakumbushwa kuwa si yale tuliyofanya ambayo yanatufanya wenye haki mbele za Mungu bali yale aliyofanya kwaajili yetu katika Kristo Yesu, ambaye ni haki yetu. Uhusiano wetu na Yesu unatufanya kuwa wenye haki mbele za Mungu Baba ambaye anatufurahia! Bwama anayeishi ndani yetu anayefanya kazi ndani yetu anatufanya tuwa watu wasio laumika mbele zake. Haki yeke inatufunika kama vazi la haki lililowekwa juu yetu. Hali yetu ya dhambi bado ipo lakini imefunikwa na utakatifu wa Kristo.

## SOMO LA TANO ~ Sehemu ya 2

**ZOEZI**:
Tukirudi kwa 2 Samweli 22…
1. (Mstari 26-27a) Mungu anajionyesha kuwa kuwa ______________________________________,
___________________________________, na ________________________________ kwa Mwaminifu asiyelaumika, na msafi. Anajionyeshaje ,kwa wasio wanyoofu (mstari 27b)?
_________________________________________________________________
Unaokoa __________________________ lakini ________________________yako iko kwenye
_______________________________________________ kuwaweka chini (mstari 28).
2. Mistari 29, 31, na 32 hutumia maneno matatu kuongea na Mungu.. Mambo hayo matatu ni yapi?
a. _________________________________________________________________________
b. _________________________________________________________________________
c. _________________________________________________________________________
3. Ni Mungu anitiaye nguvu. Kupigana vita na maadui inahitaji nguvu. Ni vita na niko tayari kwa _________________ (mstari 35) na ________________( mastari 36).

Unaniweka tayari kwa vita na kunipa ushindi You. Unashusha. ______________________________________________________(mstari 36b).
4. Kwasababu Bwana ananipa nguvu kwaajili ya vita ( mstari 40) inatokea nini kwa adversaries, my enemies, my foes (verse 40b-43)?
__________________________________________________________wangu
5. Katika mstari 44-46 unasikia moyo wa mfalme?
________________________________________________________________
6. Daudi anamsifu Bwana! Anaishi! Anapaswa kuinuliwa! Ananilipia kisasi (matari 49a) ___________________________________________________________

## MASWALI YA MATUMIZI:

- Bwana ananiweka huru kutoka maadui zangu. Ukweli unaleta tofauti gani katika maisha ninayoishi?

________________________________________________________________

## SALA:

Mimi pia nantaka kukusifu, Ee Mungu wangu kwa mambo yasiyohesabiwa uliyonifanyia. Ninataka kuimba sifa zako kwa kuwaelezea wengine. Chochea mawazo yangu nikumbuke yote uliyonitendea, kwa shukrani nilisifu jina lako:

______________________________________________________________________

Utawala wa Daudi ulikuwa mzuri zaidi katika historia ya Israeli. Daudi alikuwa mwanamume ambaye alikuwa moyoni mwa Mungu (Mdo 13:22) na alifurahia upendeleo wa Mungu (Mdo. 7:46) maisha yake yote. Sasa ni mkubwa na kuwa na miaka mingi (1 Wafalme 1:1). Wakati umefika mfalme mwingine anatiwa mafuta.

## KAZI YA KUFANYA:

Saoma 1 Wafalme 1.

- Nani anamweka kuwa mfalme
- Hii ina maana gani kwa Berisheba and Sulemani?
- Daudi anafanya nini?
- Nani anatawala kama mfalme wa Israeli?

## FUNDISHO:

Kutok kwenyesomo lako la 1 Wafalme 1 uanajifunza kuwa Adonijah, Mtoto wa Daudi wa nne (2 Samweli 3:4),

Amejitangaza mwenyewe kuwa mfalme. Pamoja na hayo nabii Nathani anamwambia Berisheba maana ya jambo hili lina maana gani kwake na kwa Sulemani na kumshauri jinsi ya kuokoa maisha yake na ya Sulemani (1 Kings 1:11-14). Kwa ujasiri alimwendea mfalme Daudi na kukumbusha ahadi yake kuwa Sulemani angekalia kiti cha ufalme cha baba yake Daudi

(mstari 17). Kuhani Zadoki alimtawaza Sulemani (mstari 39). Adonija aliposikia kuwa baba yake amemtangaza kuwa mfalme na aliposikia vifijo vya watu wote mbele ya Sulemani na kwamba Sulemani angeokoa maisha yake. (mstari 49-51). Sulemani alipeleka ujumbe kwa Adonija (mstari 52-53). “Ikiwa atajionyesha kuwa mtu anayestahili, na siyo nywele za kichwani mwake ataanguka ardhini; na ikiwa atakutwa na uovu atakufa .”

## KUCHIMBA KWA KINA:

Kabla Daudi hajafariki (2 Kings 2) alimwagiza Sulemani kuwa na nguvu na kuheshimu sheria na amri zilizoandikwa katika Sheria ya Musa. Alimwonya kuhusu Yoabu na Shimei lakini alimtaka aonyeshe ukorimu kwa wana wa Barzillai aliyebaki mwaminifu kwake alipomkimbia Abusolomu.

Uovu ulionekana ndani ya Adonija Adonijah alipoomba kumuoa Abishag, bikira aliyemuhudumia mfalme Dausi (1Wafalme 1:1-4). Ombi la Adonija lilikuwa jaribio linguine la kupata utawala. Aliyemiliki nyumba ya vijakazi wa ndiye aiyekuwa na haki ya kurithi kiti chas utawala. Adoniya alikuwa mtoto wa kifalme kufariki—mtoto aliyezaliwa na Berisheba, Amnoni, Absolomu, na sasa Adonija. Daudi alitaka katika 2 Samweli 12:6 kuwa malipo ya kuchukua kondoo yalikuwa maria nne. Malipo yalilipwa kwa ukamilifu.

Aliyefuata kufariki alikuwa Yoabu (mstari 28-34). Benaiah alichukua nafasi ya kamanda wa jeshei Joabu. Zadoki alichukua nafasi ya Abiathar kama kuhani. Mwisho, Shimei kutoka ukoo wa familia ya Saul aliangushwa wa movu yote aliyomfanyia Daudi. Sasa ufalme ulikuwa umeimarishwa mikononi mwa Sulemani (mstari 46b).

Kwahiyo majina mengi! Majina mengi yanayofahamika! Siyo majina yaliyozoeleka kama Tom, Diki, na Hari. Kutunza majina hayo yanapata shida zaidi kwa mila kutoka utawala wa Sauli kwenda kwa Daudi na sasa toka kwa Dauli kwenda wa Sulemani. Majina muhimu yanajumuisha:

- wana wa Daudi (Amnoni, Absalomu, na Adonija),
- makuhani (Abiathari na utawala wa Daudi na Zadoki wa utawala wa Sulemani), na
- makamanda wa jeshi (Abneri pamoja na Sauli, Yoabu pamoja na Daudi, na sasa Benaia pamoja na Sulemani).

Usikate tamaa. Usishushwe. Endelea mbele na uanze kumfahamu mfalme Sulemani.

# SOMO LA TANO ~ Sehemu ya 3

## KAZI YA KUFANYA:

Katika sehemu hii ya habari tunakwenda kwenye kitabu cha Mambo ya Nyakati cha pili. Habari nyingi zilizoelezewa katika Wafalme wa kwanza na wapili pia yako katika Mambo ya Nyakari wa kwanza na wa pili. Soma 2 Nyakati 1:1-17. Kumbuka: Unaweza kuchagua kusoma koo katika 1 Wafalme 3:4-15.

## ZOEZI:

1. Sulemani na hawa wote walikusanyiak Gibeoni. Kulikuwa na nini ( mstari 3)?

________________________________________________________________

2. Sanduka la Agano ambalo Daudi alileta toka Kiriathi Jearimu lilikuwa wapi (mstari4)?

________________________________________________________________

3. Altare ya shaba ilikuwa mbele ya Hema ya kukutania iliyokuwa Gibeoni. Sulemani alifanya nini.(mstari wa 6)?

________________________________________________________________

4. Kulitoke nini usiku ule? Bwana alimwambia nini Sulemani (mstari 7)?

______________________________________________________________________

5. Sulemani alijibu nini ( mstari 8-10)?

______________________________________________________________________

6. Mungu aliitikia nini (mstari 11-12)?

______________________________________________________________________

7. Ni nini baadhi ya utajiri aliokuwa nao Sulemani wakati wa utawala wake kwa Israeli (mstari 14-17)?

______________________________________________________________________

**MATUMIZI**:
Mtu hawezi kusaidia isipokuwa kufurahia kiongozi anayetanguliza watu wake. Badala ya kuomba vitu kwaajili yake, Sulemani aliomba hekima na ufahamu ambao ungemwezesha kuongoza watu wa Mungu. Hekima ni ufahamu. Ufahamu ni kujifunza na kufahamu Neno la Mungu. Hekima ni uwezo wa kutumia ufahamu wa Mungu na Neno lake katika mazingira ya kila siku.

1. Tunaweza kujifunza kutoka kwa Sulemani. Sulemani alijua jambo linalotakiwa kufanya kazi ya Mungu aliyoitiwa kufanya. Katika Kitabu cha Agano la Jipya , akitabu cha Yakombo kilihimiza kuomba kwaajili ya hekima. Andika Yakobo 1:5 –

______________________________________________________________________

2.Tumepewa fursa ya kuomba lolote ambalo tungetaka Mungu atupatie. Kwanini kuomba hekima?

______________________________________________________________________

3. Je uko katka nafasi ya uongozi katika maeneo ya nyumbani kwako? Shuleni? Kazini? Katika jamii? Uko kanisani? Ni katika mazingira gani ambayo Hekima ya Mungu itakuwezesha kuongoza katika hali inayompendeza?

